

Fred Simiyu Wanjala

Department of Kiswahili and Other African Languages
Kibabii University
E-mail: wsimiyu@kibu.ac.ke

Abstract

This study focuses on the role of multigenerism in African Oral Literature in performance. On this prism, the research used Bukusu's embalu and Makunduchi's mwaka kogwa rituals as platforms and springboards to unravel the importance of multigenerism nature of African Oral Literature in performance; a lacuna that has not been fully exploited. The study has underscored the fact that, African Oral Literature should not be analysed as independent units. The research findings show that, the two rituals are constructed and empowered to perform their functions through a continuous interplay of inseparable genres which constantly interrelate through processes like intertextuality, dialogism, genre eclipsing, generic chorusing and genre reconstruction, while in performance. These genre dynamics helps these two rituals to perform their functions through several ways; which this paper discusses in detail. These findings confirms what Senkoro (2011a) alludes that genres in African Oral literature refuses to be itemised into independent units. The research makes a contribution towards improving the approaches used in analysing African Oral Literature with the multigeneric reality in mind; contrary to the usual approaches, (Bayo 2012), (Okporoboro 2006), (Ogumbiyi 1988) and (Kubik 1977). This research was conducted in Bungoma County and Zanzibar Island, where the researcher to collect songs, praise poetry, dirges and chants that were performed in the two rituals. A blend of Ethnopoetics and Emic Theory guided the collection and interpretation of data about the multigeneric nature of African Oral Literature. Ethnopoetics helped the researcher to collect data by mingling and interacting with the study community, while the Emic Theory guided the researcher into utilizing the insiders' views on the nature of the study community's oral literature. An Ethnomethodological approach which included participation,

observation and interviews was applied in the data collection. Data interpretation and analysis was done using the interpretivism approach to give a descriptive analysis guided by the research objectives and the tenets of the two theories.

Utangulizi

Utafiti uliofanywa kuhusu mwingilianotanzu katika mivigha ya *embalumwaka kogwa* umedhihirisha kuwa, tanzu mbalimbali katika mivigha hii huchanganyikana wakati wa utendaji, na kwa hivyo, hazipaswi kuwekewa mipaka ya kudumu. Tanzania hizi ni pamoja na nyimbo, malumbano ya utani, majigambo, maghani, methali, misemo, tarihi, visasili, khurafa, mighani na misimu. Baada ya kubainisha uwepo wa mwingilianotanzu katika mivigha ya *embalu na mwaka kogwa*, makala hii inachunguza nafasi ya huu mwingiliano wa tanzu katika uamilishaji wa mivigha *embalu na mwaka kogwa*. Hii ina maana kuwa, uchambuzi katika makala hii unalenga kubainisha namna ambavyo mwingilianotanzu huu ni nguzo muhimu katika kuiwezesha mivigha ya *embalu na mwaka kogwa* kutekeleza majukumu yake. Kwa hivyo basi, makala imebainisha kuwa, mwingilianotanzu, (hali ambayo hujitokeza ama kwa fanani kujua au kutojua), huiwezesha *embalu na mwaka kogwa* kutekeleza kazi yake kupitia kwa namna mbalimbali:

Kujenga Mivigha za *Embalu na Mwaka Kogwa*

Fanani katika mivigha ya *embalumwaka kogwa* hutumia kongoo la fasihi simulizi ya jamii za Babukusu na Wamakunduchi kama marejeleo yake. Ndani ya kongoo hili, kuna tanzu zenye asili tofauti, zilizotungwa na watu tofauti, katika miktadha tofauti na kurejelea matukio tofauti huletwa pamoja. Kwa mfano, fanani katika majigambo yanayotolewa katika hatua ya upakaji wa tope maalum (*khulonga*), ndani ya mivigha ya *embalu* anatumia tanzu kama vile methali ya *Kitimule*, kisasili cha *Chetambe* na kilecha *Mango* ndani ya majigambo yenyewe. Hizi ni tanzu ambazo zina asili tofauti kwani kila moja ilibuniwa kutokana na matukio tofauti na inawezekana kabisa kuwa tanzu hizi zilibunwa na watu tofauti. Methali ya *Kitimule* ilibunwa kutokana na tukio la Babukusu la kudhani kuwa watu kutoka nasaba ya Bayumbu walikuwa wala watu; kisasili cha *Chetambe* kilibunwa kutokana na vita kati ya wakoloni na Babukusu; nacho kisasili cha *Mango* kilitokana na matukio yaliyojiri wakati wa mapigano kati ya *Mango* na nyoka mla watu (*Yabebe*), pamoja na kule kutahiriwa kwa *Mango* mwenyewe kama mwanaume wa kwanza kutahiriwa miongoni mwa Babukusu. Tanzania hizi zinaletwa pamoja na fanani ili kuunda

fani na maudhui ya haya majigambo. Kuhusu hili, Chesaina (2003) anasema kuwa, ngano ndio utanzu ambao ni makutano ya tanzu zingine, kutokana na uwezo wake wa kubeba tanzu zingine kwa kuzipa majukumu mapya pamoja na ngano yenyewe kujiimarisha kimuundo na kifani. Naye McCaskie (1989: 75) anadai:

Ubunaji na ubunaji-upya wa vijenzi vya *asantesem* unakaidi mipaka dhahiri ya kifasili, kwani *asantesem* ni zao la mahojiano na mazungumzo ya ndani kwa ndani *kati ya vijenzi vyake*, yanayoifanya iwe nyumbufu, changamano na yenye mianya. Hili hii huifanya ikaidi uwezekano wa kuichambua kipwekepewe, (msisitizo ni wangu).

Hii ina maana kwamba, *embalu* na *mwaka kogwa* kama mfumo timilifu ulio na miuundo dhahiri ni zao la uumbaji wa Babukusu na Wamakunduchi, unaojengwa kwa tanzu mbalimbali zinazoingiliana katika viwango (vivigha) tofautitofauti. Kuhusu hili, McCaskie (1989) anashikilia kuwa, uainishaji na *uchanganuzi* (msisitizo ni wangu) wa *asantesem* ni wa kimuktadha na wa kiutendaji. Hii ni kwa sababu, maudhui yenyewe yanategemea nyongeza na punguzo linalotokana na utendaji. Kwa kuunganisha yaliyokuwa yametenganishwa; na kwa kusema kitu kilekile kwa njia tofautitofauti, mivigha ya *embalu* na *mwaka kogwa* huibuka na muktadha changamano unowezesha maana mpya kuibuliwa huku ya jadi ikipanuliwa na kupewa sura mpya katika ulimwengu wa sasa. Barber (1991: 20) anaunga hili mkono anaposema:

Kongoo la *oriki* linalolenga mada fulani maalum, huundwa kwa fito zinazotokana na tanzu tofautitofauti. Kwa hivyo, tanzu hazina uhusiano wowote tofauti na uhusiano unaopatikana kutokana utendaji husika. Mwingilianotanzu huu unaweza kufasiliwa kwa msembo: enyi tanzu nendeni pamoja, kwa njia moja au nyingine, hata kama hamkutungwa pamoja na wala kwa lengo moja.

Maumbo ya *embalumawaka kogwa* inatokana na mifanyiko ya kingazi ya kitanzu. Utafiti huu umebainisha kuwa, mifanyiko hii ya kitanzu huanza na tanzu ndogongogo kubebwa na tanzu kubwa kiasi. Hizi tanzu ndogo ni pamoja na methali, misemo, misimu na ngano ambazo huungana ili hujenga tanzu kubwa kiasi. Tanzu zinazobeba hizi tanzu ndogondogo ni pamoja na nyimbo, maghani, malumbano ya utani, ngonjera na majigambo. Hatimaye, hizi tanzu kubwa kiasi huingiliana na kushirikiana kupitia mifanyiko mbalimbali ya kitanzu katika kujenga tanzu kuu ambazo ni *embalu* na *mwaka kogwa*. Kwa

hivyo, tanzu ndogondogo kupitia kwa tanzu kubwa kiasi hujenga maudhui na fani ya *embalu* na *mwaka kogwa*. Hii ina maana kuwa, hizi tanzu ndogondogo pamoja na tanzu kubwa kiasi zikiondoshwa, tanzu kuu hazitakuwepo. Barber (1989: 14) anachangia hili kwa kusema kuwa, matini zote hupatikana ndani ya matini nyingine kupitia mifanyiko mahuluti ya mwingilianomatini.

Kwa mfano majigambo yaliyotolewa katika jukwaa la *khulonga* (*shughuli ya kumpaka mtahiriwa tope maalum*) katika mivigha ya *embalu*, yameundwa kutokana na tanzu ndogondogo kama vile misemo: *lirango lie 'njofu (paja la tembo)*, *chinyuni chafwa (nyuni wakafa wote)*, *omwana bulilo (mtoto ni mali)*, *bang'ang'ula mafunga (ngariba watajika)*, na *engubo ya Mango (nguo ya mwazilishi wa tohara kwa jina Mango)*; methali: *rebanga Kitimule wanyoa Ebuyumbu (uliza Kitimule aliyetangulia kuifikia nasaba ya Bayumbu)*, *eng'ana ye emboko yambukhila nie mawe yambukhila (mtoto wa nyoka ni nyoka)* na *wesalila akhila webale (aliyezaa ni bora kuliko tasa)*; na kisasili cha *Chetambe*.

Katika mivigha ya *mwaka kogwa*, kuna malumbano ya utani yanayotolewa wakati wa uchomaji wa kibanda ambapo, waimbaji wanatumia methali mbili: *mkosa mila ni mtumwa* na *baniani mbaya kiatu chake dawa*, ambazo ndizo kitovu cha malumbano yao. Methali hizi zinatumiwa katika malumbano haya ya utani ili kurithisha historia na utamaduni wa Wamakunduchi. Kwa mfano, methali *mkosa mila ni mtumwa*, inatumia kwanza kusimulia kuhusu ujio wa biashara ya watumwa pamoja na kutetea uendelezaji wa mila na desturi za Wamakunduchi, ikiwemo usherekeaji wa mivigha ya *mwaka kogwa*. Kwa hivyo, mivigha hii imejengwa kwa fito za malumbano ya utani, nyimbo, majigambo, mighani na maghani yanayoshirikiana na kuingiliana kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa hakika, *embalu* au *mwaka kogwa* haiwi mivigha iwapo tanzu hizi zitaondolewa. Ikitokea hivyo, basi *embalumawaka kogwa* itasalia kuwa kovu ambalo halina muundo wala maudhui yoyote.

Mbinu ya Kuhalalisha Maoni ya Fanani

Katika jamii nyingi za Kiafrika, wazee hushikilia nafasi maalum ya kuelekeza jamii kupitia kwa maneno yao yenye busara. Busara na hekima hii inatokana na umri pamoja na tarjiba yao pevu inayotokana na wao kuishi na kuona mengi. Maneno haya ya wahenga hubeba sauti na mamlaka ya jamii nzima. Kwa hivyo, mtu yeyote katika jamii akitaka asikilizwe kwa makini, anaweza akatumia baadhi ya maneno ya wazee hawa, ambayo huhifadhiwa ndani ya tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. Tanzu hizi ni kama vile, methali, misemo

na ngano. Hii ndio maana, fanani hutumia tanzu ndogondogo katika tanzu kubwa kiasi kwa lengo la kutafuta sauti yenye mamlaka na ya kijamii ili wazo au maoni yake yaweze kukubalika kwa urahisi na jamii. Kwa hivyo, matumizi ya methali, misemo na ngano katika nyimbo, majigambo na maghani ni uingizaji wa sauti ya wahenga wanaowakilisha jamii nzima.

Kwa mfano, fanani katika majigambo ya *khulonga* (*shughuli ya upakaji wa tope maalum*) katika mivigha ya *embalu*, anatumia methali, *Rebanga Kitimule wanyoa Ebuyumbu* (*muuliza Kitimule aliyetangulia kuifikia nasaba ya bayumbu*), kuonyesha kuwa, yeye ndiye ametumwa kumuumba mtahiriwa kutokana na sifa na tajiriba yake pana. Aidha, methali hii inajinyambua na kuwa kisasili kinachoihusu nasaba ya Bayumbu. Fanani anatumia methali au kisasili hiki kutafuta sauti ya wahenga ili kuhalalisha anachokisema kupitia majigambo husika. Kadhalika, katika maghani yenye kichwa *khwamba mutalia* ndani ya mivigha ya *embalu*, fanani anatumia mighani kuhusu Elijah wa Nameme ili apate mamlaka ya kijamii ya kuweza kugundua kuwa Rais Mstaafu aliwasaidia sana Wasabaot kwa kuwaagizia zana za vita wakati wa vita kati ya Babukusu na Wasabaoti mwaka 1992. Fanani anajifananiisha na jagina anayefahamika na kuheshimika miongoni mwa Babukusu kutokana na uwezo wa kibashiri, ili walengwa waweze kumsikiliza kwa makini.

Kuonyesha Umahiri wa Fanani

Mwingilianotanzu unaweze kutumiwa kama mizani ya kupima ubingwa wa fanani husika. Hii ni kwa sababu, uhamaji kutoka utanzu mmoja hadi mwingine bila shida yoyote unathibitisha ubingwa wa fanani katika kumaizi fasihi simulizi ya Basotho pamoja na uwezo wake mkubwa wa kukumbuka, Tsui (2008). Utanzu ndani ya utanzu mwingine au unaotolewa sambamba na utanzu husika, unaweza kubainika tu kutokana na fani au maudhui yake. Hii ni kwa sababu, maneno au mishororo inayochukuliwa au kunukuniwa kutoka tanzu hizi zinazobebwa na tanzu zingine huwa sio kamilifu. Fanani, hususan wale magwiji huvunjavunja tanzu hizi kimakusudi na kuchukua vipande kutoka tanzu zingine katika ustadi wa hali ya juu. Wanaweza kuurejelea tena utanzu tajwa baadaye na kuutolea maelezo marefu au kuiachia hadhira itafakari. Kwa hivyo basi, sehemu hizi za tanzu zinaweza kujitenga na kusimamia ile maana lengwa ya utanzu husika au kutumiwa kwa namna tofauti kabisa. Kuhusu hili, Tsui (2008: 234), anasema:

Uhamaji wa fanani kutoka *thoko* (*majigambo*) hadi *sefela* (*maghani ya wachimba migodi*); *sefela* (*maghani ya wachimba migodi*) hadi *thoko* (*majigambo*) na hatimaye kutoka *thoko* (*majigambo*) hadi

mkubwa hivi kwamba ni vigumu kubainisha mipaka kati ya tanzu hizi. Mipaka inabainika tu kupitia ubainishaji wa maudhui ya kila utanzu katika fasihi simulizi ya Basotho.

Hiyo basi, fanani ambaye ana uwezo wa kutumia tanzu nyingi ndani ya utanzu mmoja huchukuliwa kama mulumbi hodari. Kwa hivyo, mwingilianotanzu hutumiwa kudhihirisha kuwa fanani husika anaelewa jamii pamoja na utamaduni wake barabara. Hali hii huifanya hadhira imsikilize kwa makini. Maitaria (2010: 15) anaunga hili mkono kwa kusema:

Matumizi ya methali zaidi ya moja katika uwasilishaji wa ushairi huweza kutumiwa kama mizani ya kubainisha umahiri na uhodari wa fanani; ni mbinu ya kuhakiki viwango vya umbuji au ubunifu wa watunzi.

Hali hii inadhiririka katika tanzu tulizochambua katika mivigha ya *embalumamwaka kogwa*. Kwa mfano, katika wimbo *wachebutang'i*, fanani anatumia methali *omwana wesecha sikolonjo silinda ekunda*, kwa maana ya, *mtoto wa kiume ndiye mhimili wa mila na desturi*. Hapa, fanani anachagua neno kuu katika methali na kulingiza katika wimbo ili kueleza namna kikundi hiki cha bamwalie kinavyothamini na kuendeleza utamaduni wao. Uteuzi na uingizaji wa neno hili linalosimamia ujumbe ndani ya methali husika unafanywa kwa ufundi wa hali ya juu ili kupitisha ujumbe uliokusudiwa pamoja na kuuwezesha wimbo uweze kuimbika. Ufundi huu wa fanani unaiwezesha mivigha ya *embalu* kutekeleza wajibu wake mbalimbali kwa wakati mmoja kupitia kwa mwingilianotanzu.

Mbinu za Kifani

Kila fanani hujitahidi kuibuka na mwingiliaontanzu uliosukwa vizuri ili kidhihirisha ubingwa wake wa kisanii. Barber (1991) anashadidia hili kwa kusema kuwa, kila utanzu katika maghani ya *oriki* umeunganishwa na tanzu zingine kwa namna ya ajabu, kwani tanzu zinachukuliana nafasi katika kukamilisha utanzu mkuu wa *oriki*. Halikadhalika, umbo na muundo katika *embalumamwaka kogwa* unatokana na uradidi na mpangilio maalum wa tanzu ambazo huathiri matendo na matukio ndani ya mivigha hii, kwa madhumuni maalum (kuweza kutekeleza majukumu yaliyonuiwa na jamii). Kuhusu hili, Semkoro (2011) anasema kwamba, tanzu huingizwa katika tanzu zingine ili kuleta mtiririko wautakao fanani, wakaunganisha sehemu na sehemu katika visa vyao.

Kwa mfano katika wimbo wa 'Shamba' tunatambua kuwa, kuna matumizi ya semi nyingi ambazo zimefuatana. Kwa mfano, kuna methali kama vile *mpunga bila kuutwanga huupati mchele wake; mtoto akililia wembe mpe*; na *kila mgombea fupa mwisho humng'oa meno*. Methali ya kwanza ina maana kuwa, ukitaka kupata kitu kizuri lazima ukihangaikie. Kitu hicho kizuri kinamithilishwa na mchele ambao haupatikani hivi hivi tu bila kufanya kazi ya kuukoboa mpunga, shughuli ambayo huchosha. Methali ya pili inalenga kuwaasa wanajami kuwa, wanapokumbana na watoto wasiozingitia maelekezo ya wazazi wao, wanapaswa kuwaacha maana hatimaye watapata shida. Aidha, methali ya tatu inabeba ujumbe kama ule wa methali ya pili.

Kwa hivyo, tanzu ndogondogo hutumiwa kama matofali ya kujenga tanzu kubwa kiasi. Chesaina (1997) anashadidia rai hili kwa kudai kuwa, inawezekana kabisa kuwa, nyimbo hutumiwa ndani ya hadithi kama mbinu ya ukando katika drama. Chesaina (1997: 19) anachangia hoja hii anapodai kuwa:

Ingawa kila utanzu una sifa zake, na mahali pamoja na muda wa kutolewa, tanzu hizi wakati mwingine huingiliana. Utanzu wa hadithi ndio una uwezo mkubwa wa kubeba tanzu zingine katika utendaji. Tanzu zinazobebwa na hadithi huiongezea ufasihi wake pamoja na kuisaidia iweze kutekeleza wajibu wake vizuri zaidi.

Kusisitiza na Kupanua Wigo wa Maudhui

Mwingilianotanzu unachangia pakubwa katika kuibua maudhui yenyewe na kuonyesha umuhimu wake katika tanzu kuu za *embalu* na *mwaka kogwa*. Tsui (2008) anaunga hili mkono kwa kusema kuwa, fanani anatoka katika *thoko* na kiungia katika utanzu wa *sebeko* kwa lengo la kutaka kupitisha ujumbe wa ziada. Kwa hivyo, hali hii ya mwingilianotanzu humsaidia fanani kupitisha ujumbe mbalimbali kwa wakati mmoja na ndani ya utanzu mmoja. Naye Tonkin (1989: 42) anashadidia hili kwa kudai kuwa, baadhi ya tanzu huchukuliwa kama nyenzo zinazobeba taarifa maalum.

Kwa mfano, katikamajigambo ya *khulonga* (yanayotolewa wakati wa kupaka mtahiriwa tope maalum) yanabeba tanzu kama vile misemo: *lirango lie 'njofo* (*paja la tembo*), *chinyumi chafwa* (*nyuni wakafa wote*), *omwana bulilo* (*mtoto ni mali*), *bang'ang'ula mafunga* (*ngariba watajika*) na *engubo ya Mango* (*nguo ya mwazilishi wa tohara kwa jina Mango*); methali: *rebanga Kitimule wanyoa Ebuyumbu* (*uliza Kitimule aliyetangulia kaifikia nasaba ya bayumbu*), *eng'ana ye emboko yambukhila nie mawe yambukhila* (*mtoto wa nyoka ni*

nyoka) na *wesalila akhila webale* (*aliyezaa ni bora kuliko tasa*); na kisasili cha *Chetambe* (*jina la sehemu ambapo Babukusu waliuwawa sana wakati wa vita vyo kupigania uhuru*). Methali ya *rebanga Kitimule wanyoa Ebuyumbu* hutumiwa kwa lengo la kuwaasa walengwa watafute ushauri wa waliowatangulia katika jambo husika kabla ya kulifanya naye *eng'ana ye emboko yambukhila nie mawe yambukhila*, ikiwaasa watahiriwa wafuate nyayo za wazazi wao katika kufanya mambo mzuri.

Matumizi ya semi hizi nne yanalenga mambo manne tofauti: ujitofuatishaji na ujitambuaji wa Babukusu; umuhimu wa ujasiri; umuhimu wa watoto katika ndoa; ubingwa wa nasaba ya Bayemba katika kazi ya ungariba; na umuhimu wa jagina kwa jina Mango katika maisha ya ukubwani miongoni mwa Babukusu. Kuhusu hili, Kalogirou na Vasso (2012) wanasema kwamba, wingi wa matini ndani ya matini moja huzalisha maana tofautitofauti zinazohusiana.

Hatimaye kisasili cha *Chetambe* kinatolewa kupitia kutajwa tu kwa jina la sehemu ambapo mapigano makali ya katafuta uhuru yalitokea, ili kuwakumbusha watahiriwa matukio ya kihistoria na umuhimu wake katika maisha ya sasa. Utajaji wa aina hii unabainishwa pia na Chesaina (2003) anayedai kuwa, wakati mwingine, jina la shujaa maarufu katika jamii hutajwa katika wimbo, *hivyo kuingiza mighani ndani ya wimbo husika*, (msisitizo ni wangu). Aidha, msembo wa kwanza, una maana kuwa, msemaji alistahimili kisu kwa ushujaa mkubwa hadi Mungu akamtunuku kwa kuwaua nyuni wote ili watu waweze kupata kitoo kwa ajili ya kusherekea ushindi huo. Nayo methali ya kwanza inamaanisha kuwa, mtoto wa nyoka anapaswa kuwa nyoka na si vinginevyo. Hii inatumiwa kumrejelea mtahiriwa anayepaswa kufuata nyayo za muumba wake katika kustahimili kisu.

Methali ya pili ina maana kuwa, mtahiriwa anahimizwa awe mtaratibu kwa kujiepushia tabia ya kuwa na pupa, kwani, Mbakara aliyekuwa na pupa alikula vibachi. Jina Mbakara lina maana ya mtu ambaye anapenda kufanya mambo kwa haraka haraka bila uangalifu wowote. Kwa hivyo, muumbaji anamdhihirishia mtahiriwa kuwa, *mwenye pupa hadiriki kula tamu*. Fanani anatumia msembo na methali hii katika ubeti wa pili kwa tanzu hizi kutenguana, kuingiliana kimatini, kusemezana na kuingiliana kukorasi. Haya yote yanasemwa na fanani kwa wakati mmoja kupitia mwingilianotanzu. Kuhusu wajibu huu, Herman (2011: 80) anasema:

Katika ubunifu wa masimulizi, suala la mwingilianomatini *badala ya mwingilianotanzu*, humfanya msikilizaji aweze kuwa na uwezo wa kupokea mambo mengi kwa wakati mmoja, (msisitizo ni wangu).

Kuhusu hili, Namulandah (2011: 36) anashadidia hali hii ya mwingilianotanzu kwa kusema:

Nyimbo ni sehemu muhimu sana ya ngano. Hutumiwa kuboresha usimuliaji; kama kuingo cha matukio katika msuko husika; hutambulisha au kuzua taharuki na kuondoa uchovu wa masimulizi. Wakati mwingine, nyimbo ndio maudhui wakati masimulizi hubeba maudhui yenyewe.

Kutoa Muhtasari na Majumuisho

Tanzu ndogondogo hutumika kama majumuisho ya maudhui ndani ya tanzu kubwa kiasi na tanzu kuu. Hali hii hudhihirika kupitia namna mbalimbali: Kwanza, kuna baadhi ya tanzu ambazo pia zinatumiya tanzu zingine kama anwani ili kudokeza yaliyoma kwa ufupi. Maoni haya yanungwa mkono na Sengo na Wengine (1987) wanaposema kwamba, kuna hadithi fupi kadha na mashairi mengi ambayo hutumia methali kama vichwa au kama semi zenye hekima zinazoongezea uzito katika maudhui. Katika kazi yetu, maghani ya *khwamba mutalia*, majigambo ya *euno*, wimbo wa *Pembe* na ule wa *Shamba* unadhihirisha matumizi ya tanzu zingine kama anwani. Kuhusu hili, Maitaria (2010: 109) anasema:

Ushairi *waukimeani* ule ambao hutumia methali katika anwani yake.

Aidha, kwa kuwa semi hizi huwa zimezoeleka, matumizi yake hutoa muhtasari wa maelezo marefu ndani ya utanzu husika. Senkoro (2011) anashadidia hoja hii kwa kudai kuwa, wimbo hutumiwa ndani ya ngano ili kuleta msisitizo wa jambo fualani ambalo mtambaji analiona kuwa lina umuhimu...pia unaweza kutumiwa kama njia ya kuondoa uchovu pale ambapo msanii anang'amua kuwa, ametoa maelezo marefu mno ya kinathari. Naye Chesaina (1991) anasema kwamba, methali hutumiwa katika ngano kwa ajili ya kuhitimisha ngano husika au kutoa muhtasari wa mafunzo ndani ya ngano hizo.

Pili, tanzu hutumiwa kama mkarara au kiitikio cha tanzu zingine ili kutoa mukhtasari wa yaliyomo. Urudiajirudiaji wa sehemu fulani ya utanzu husika (mkarara au kiitikio) kwa lengo la kuisisitiza kinachoelezwa huwarudisha waimbaji nyuma au kuwapeleka mbele ya tukio kwa namna ya utabiri. Matumizi yake basi, yanamsaidia fanani kubainisha kitovu cha kazi yake kwa

njia ya kiitikio. Kwa mfano, msembo *waeuno* unatumiwa kama mkarara katika maghani ya *euno* ndani ya *embalu* ili kufupisha maelezo ambayo yangetatiza ughanikaji wa maghani haya. Ndani ya mkarara huu, wanajamii wanajisahili na kukata kauli ya kukubali kuendeleza na kudumisha mila ya *embalu*. Mkarara huu ni kama kiitikio kwa maneno anayotoa fanani katika mishororo mbalimbali. Msembo huu hutumika ama na hadhira kuhitimisha mishororo husika; mara nyingine unatumiwa na fanani kuonyesha mwazo wa beti husika; au kutumiwa na hadhira kuhitimisha ubeti husika unaobeba mishororo kadhaa. Vilevile, uradidi huu huchangia katika kuleta uimbikaji wa wimbo haswa kuhusiana na mapigo yanayotokana na mizani na vina. Uradidi wa maneno, mishororo au kipande fulani huisaidia hadhira kujinasibisha na utanzu unaotolewa ili iweze kujumuika katika utendaji. Kwa ujumla, msisitizo huu wa yaliyomo katika tanzu mbalimbali unasisitiza pia majukumu ya mivigha ya *embalu* na *mwaka kogwa*, hivyo kuisaidia kutekeleza wajibu wake vizuri zaidi.

Kufikirisha Jamii

Fanani mtajika hutumia tanzu mbalimbali ili kuzua taharuki miongoni mwa hadhira yake. Hapa, fanani anaweza kuanza kuimba wimbo halafu ghafla, anaacha na kuanza kutongoa hadithi, labda, kisasili na kabla ya kukamalisha utongoaji, akataja methali na kuhitimisha na majigambo. Kila utanzu unazua hamu ya kutaka kujua zaidi, kwa kukoleza maudhui makuu. Fanani anatumia tanzu hizi kubainisha ama mandhari yaleyale au tofauti yanayosisitizwa na tanzu zingine kupitia mwingiliano wa korasi. Hili hii huifanya hadhira iwe makini kwa kutafakarishwa kuhusu jambo moja kwa undani au mambo mengi yanayotokana na kukaribiana kwake.

Matumizi ya tanzu ndogondogo ndani ya utanzu mkubwa, huwa na lengo la kuipumzisha hadhira. Kwa hivyo, utanzu unaotumiwa na utanzu mwingine huwa kama kituo cha mapumziko kwa hadhira. Hadhira hupewa fursa ya kutafakari kuhusu yaliyosemwa na fanani na kujiandaa zaidi. Kuhusu hili, Maitaria (2010: 114) anasema:

Methali ya katikati huifanya hadhira kuwa na kipindi cha kupumua au wasaa wa kuruhusu ubongo kutafakari mawazo yaliyoibuliwa na kuuweka tayari kupokea mawazo mapya.

Kwa mfano, katika majigambo ya *ebukhocha* (*majigambo yanayotolewa kwa mjombake mtahiriwa*), fanani anatumia methali zaidi ya moja. Kadhalika, katika wimbo wa *sioyayo*, kuna matumizi ya methali tatu katika ubeti wa mwisho: *kamaramba kaluma amwene siaki*, kwa maana kwamba, *nyigu*

walimuuma mwenyewe ghala; Olinda embalu Oli olinde 'ngwe yenye maana ya ikabili embalu kana kwamba unaikabila chui; na Onyindalila oli okhama linani kwa maana ya vumilia kama mtu anayekana zimwi. Halikadhalika, katika malumbano ya utani katika mwaka kogwa, waimbaji wanatumia methali mbili: *mkosa mila ni mtumwa na baniani mbaya kiatu chake dawa.*

Aidha, katika nyimbo za mwaka kogwa, kuna matumizi ya msemu na misimu zaidi ya moja: *ngozi kwa ngozi, kipindu pindu pindukia na nyama yangu haupati*; pamoja na matumizi ya misimu: *tutombane hadi tukwete na kutuzingua*. Vilvile, fanani katika maghani ya *euno*, ametumia methali tatu: ya kwanza ni *Murimba kufutarira nisio kulia*, yenye maana kuwa, *nyuni aina ya murimba hulipa mgongo windo lake kwa unafiki mkubwa*. Unafiki huu huwa mtego ambao huteguliwa kwa kuligeukia na kulinasa windo husika kwa ghafla. Methali ya pili ni, *Embulu okinyolela khumasifwa*, yenye maana kuwa, *mnyama aina ya embulu anapenda sana machicha na hivyo, utanapotaka kumnasa unatumia machicha*. Methali ya tatu ni *lisondo liekhukhwilakho liarafua liakhila* yenye maana, *uchungu wa kutahiriwa kwa mara ya pili kwa kutoa kipande cha ngovi kilichosahaulika ni mkubwa mno*. Matumizi haya ya semi nyingi ndani ya tanzu zingine yanalenga kuwafikirisha wanajamii kuhusu dhima ya mivigha ya *embalumwaka kogwakwa* ujumla. Semi hizi zinawafanya wanajamii kutafakari kwa kina kuhusu haja kuendelea kushiriki katika utamaduni huu hata katika ulimwengu huu wa sasa. Kuhusu hili, Chesaina (1997: 19) anasema:

Wimbo huwa kama chachu kwa fanani na hadhira kuendelea kushiriki katika matendo husika ili kuendeleza maudhui ya hadithi hiyo.

Kueleza na Kurithisha Historia

Unukuzi unaotokana na tanzu za kihistoria husaidia jamii kuendelea kuhifadhi na kurithisha utamaduni wake kwa vizazi vipya. Kupitia kwa unukuzi na urejeleaji wa matini za zamani, fanani anaunganisha vizazi vinavyopatikana katika nyakati tofauti kwa mujibu wa mpito wa wakati. Fanani anafanya hivyo kwa kupatanisha na kuhusisha matukio ya sasa na yale ya zamani. Kuhusu haya, Barber (1989) anasema kuwa, matini za jadi zina mvuto fulani unaolekeza utunzi na utolewaji wa tanzu za leo. Aidha, usasa unabainika kupitia tanzu za leo, ila zinaporithishwa na kuhifadhiwa, zinakuwa sehemu ya jadi. Naye White (1989) anasema kwamba, uimbaji wa maghani simulizi ni njia moja ya kuikubali historia, na kuondokana nayo wakati huo huo. Uhamaji

huu unamsaidia fanani kutembea na hadhira yake kutoka katika usasa huku ikiwapeleka kwenye ukale na kuwarudisha kwenye usasa kwa wakati huo huo. Kwa mfano, ingawa lengo la fanani wa wimbo wa *chebutang'i* sio kutongoa kisasili cha wanachama wa kikundi cha bamwalie, anataja asili na nasaba hizi kwa lengo la kuonyesha upekee na uteule wa kikundi hiki. Hapa, lengo sio kutaja nasaba husika, bali kubainisha mahusiano yanayowaweka pamoja Bamwalie. Anajikuta akiwasimulia hadhira ya sasa asili ya desturi hii pamoja na wanachama wake wa tangu jadi. Hili linachangiwa na Barber (1989) anaposema kuwa, maghani ya *oriki* hutolewa sio kama tukio au kitendo tu, bali kama utendaji wa kiusemezano ambapo mhusika asiye bainika waziwazi hutekeleza wajibu muhimu. Utendaji wa *oriki* humsaidia fanani aweze kudhihirisha uleo kwa kutumia matofali ya ukale lakini sio kuonyesha ukale katika usasa. Kadhalika, malumbano yanayotewa wakati wa uchomaji wa kibanda, hutumiwa kuelezea dhima ya *mwaka kogwa* pamoja na asili ya makundi haya mawili ya Wamakunduchi: wa kaskazini na wa kusini. Historia hii inatolewa kwa madhumuni ya kushindana na hata kuikumbusha jamii nzima kuhusu asili ya mgawanyiko pamoja na asili ya utamaduni wa Wamakunduchi. Hii ndio maana Wanjiku na Mutahi (1988) wanashikilia kuwa, kupitia kwa utendaji, fanani hubainisha matamania, hamu, matumaini, wasawasi na falsafa ya jamii yake pamoja na kuandika historia yake.

Aidha, mwingilianotanzu unamwezesha fanani kuvunja kingo zinazotenganisha udhahania na uhalisia. Hapa fanani anatumia tukio linalojiri katika jamii na kuliunganisha tukio ambalo lililotokea zamani. Huenda tukio la zamani limebaki kama kisa kisichokuwa na uhalisia wowote kutokana mpito wa wakati. Katika hali hii, fanani anawakumbusha kuhusu kichotokea zamani kwa kukihusisha na kinachotokea sana hivi. Chesaina (1997) anateua kauli hii kwa kusema kuwa, wakati mwingine tukio la kihistoria ndani ya hadithi linaweza kutajwa katika wimbo; kwa kutaja jina la jagina ili kuwamotisha fanani na hadhira. Naye White (1989) anaunga mkono jadi hii kwa kusema kuwa, fanani mzuri ni yule anayedhihirisha umahiri katika kuoanisha yaliyopita na yaliyopo. Kwa kufanya hivyo, watakuwa wanajaribu kuchora ramani zinazotokana na tajiriba yao kwa kusoma ramani za jadi. Kwa mfano, katika wimbo wa *wasioyayo*, fanani anataja jina la Mango ambaye ndiye jagina maarufu sana kuhusiana na masuala ya *embalu* miongoni mwa Babukusu. Hapa, fanani anaikumbusha jamii kuhusu matukio ya kishujaa aliyoyafanya Mango kwa kuyalinganisha na tendo la kishujaa la kupambana na ngariba mbele ya jamii nzima.

Kadhalika, urejeleaji wa tanzu za kale katika tanzu za kisasa unaonyesha kuwa, utunzi wa kale ni jiwe la pembeni ambalo linategemewa sana na watunzi wa leo. Urejeleaji huu ni ushahidi tosha kuwa, fanani wanaheshimu ukoko wanaoupata katika tanzu za zamani zinazobeba hekima ya wahenga. Hii ni kwa sababu, unukuzu huu humsaidia fanani kutumia tanzu za zamani kama mhimili unomwezesha kuibuka na tungo mpya au kuupa usasa utanzu wa kale ili kuusasaisha. Barber (1991) anakubaliana na kauli hii kwa kusema kwamba, kupitia utendaji, tanzu hunyambuliwa na kutungwa upya ili kuhifadhi ukweli fulani kuhusu jamii. Aidha, utendaji wake huwakilisha ukale katika usasa ili kudhihirisha uhusiano-tegemezi kati ya leo na jana. Kwa mfano, kulingana na simulizi tulizopata uwandani, maghani ya *khwamba mutalia* yanayotolewa katika *embalu*, yalizaliwa mwanzoni mwa karne ya 21 kutokana kukarabati wimbo wa *khwamba mutalia* ambao ulipigwa kwa mara ya kwanza mwaka 1948. Hili linaungwa mkono na White (1989) kwa kusema kuwa, fanani mzuri ni yule anayedhihirisha umahiri katika kuoanisha yaliyopita na yaliyopo. Kwa kufanya hivyo, watakuwa wanajaribu kuchora ramani zinazotokana na tajiriba yao kupitia kwa usomaji wa ramani za jadi.

Kuchangamsha Hadhira

Fanani hutumia tanzu zaidi ya moja katika uwasilishaji wa utanzu mkuu ili kuondoa uchovu na kuteka hisia za wasikilizaji wake ili watamani kumsikiliza zaidi na zaidi. Maelezo ya Bukenya na Wenzake (1997:71) yanaunga mkono ukweli huu:

Nyimbo, maghani na semi zinatumiwa kuisisimua hadhira ili iweze kushiriki katika utendaji wa ngano inayotongolewa.

Naye Chesaina (2003) anasema kwamba, katika utongoaji wa hadithi, vitendawili hutumiwa kama chachu ya kuisisimua hadhira. Fanani ambaye anafanikiwa kufanya hivyo bila kuathiri mtindo na muwala wa utanzu mkuu hufanikiwa kupata umaarufu miongoni mwa wanajamii. Barber (1991) anaunga mkono hili mkono kwa kusema kuwa, fanani mtajika wa *oriki* ataibua na kujaza mapengo ndani ya utanzu anaowasilisha kwa kutumia tanzu zingine ili kuondoa uchovu miongoni mwa hadhira. Urudaji wa sehemu fulani fulani za matini tofauti huendeleza mtagusano kati ya hadhira na msimulizi, Wamitila (2008). Unukuzi huu wa aina tofauti ya tanzu katika utanzu unaotolewa huongeza ladha. Kwa hivyo, fanani anasisimua hadhira yake kwa uwezo wake wa kutumia tanzu nyingi ndani ya utanzu mmoja mkuu kwa wakati mmoja.

Hitimisho

Makala hii inadhiri hii kuwa mwingilianotanzu uliobainishwa katika mivigha hii unaisaidia kuibuka na uwezo wa mwingiliano-majukumu unaotekelezwa kupitia namna mbalimbali: kujenga mivigha ya *embalu* na *mwaka kogwa*; mbinu ya kuhalalisha maoni ya fanani; kuonyesha umahiri; kuisitiza na kupanua maudhui; kutoa muhtasari na majumuisho; kufikirisha jamii; kueleza na kurithisha historia; na kuchangamsha hadhira. Njia hizi anuai huiwezesha mivigha ya *embalumwaka kogwa* kutekeleza majukumu yake mbalimbali kwa wakati mmoja.

Marejeleo

- Barber, K. (1989). "Interpreting *Oriki* as History and as Literature." Katika: K. Barber na P. F. Farias (Wah), *Discourse and its Disguises: The Interpretation of African Oral Text*. Birmingham: Centre of West African Studies, Uk 78-97.
- Barber, K. (1991). *I Could Speak until Tomorrow: Oriki, Women and the Past in a Yoruba Town*. Edinburgh: Edinburgh University Press.
- Bukenya, A. na Wengine (1997). *Oral Literature; A Senior Course*. Nairobi, Longhorn.
- Chesaina, C. (1991). *Oral Literature of the Kalenjin*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Chesaina, C. (1997). *Oral Literature of the Embu and Mbeere*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Herman, L. (2011). "Dhima ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili." Katika: Malangwa, P. S. na L. H. Bakize (Wah), *Kioo cha Lugha*. Dar es Salaam: TATAKI, uk 102-140.
- Kalogirou, T na E. Vasso. (2012). *Building Bridges between Texts: From Intertextuality to Textual Reading and Learning*. Athens: Kapodistrian University of Athens Press.
- Maitaria J. N. (2010). "Methali kama Fomula ya Uwasilishaji wa Ushauri wa Kiswahili: mfano wa Mashairi ya Abdilatif Abdalla." Katika: P. S. Malangwa na L. H. Bakize (Wah), *Kioo Cha Lugha*. Dar es Salaam: TATAKI, uk 78-88.

- McCaskie, T. C. (1989). "Asantesem: Reflections on Discourse and Text in Africa." Katika: Barber, K. na P. F. Farias (Wah), *Discourse and it's Disguises: The Interpretation of African Oral Text*. Birmingham: Centre of West African Studies, uk 67-70.
- Namulundah, F. L. (2011). *The Bukusu of Kenya: Folktales, Culture and Social Identities*. Carolina: Carolina Academic Press.
- Sengo, T. S. Y. na Wengine. (1987). *Fasihi Simulizi: Sekondari na Vyuvo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: Kauttu Ltd.
- Tonkin, E. (1989). "Oracy and Disguises of Literacy." Katika: K. Barber, na P. F. Farias, (Wah), *Discourse and it's Disguises: The Interpretation of African Oral Text*. Birmingham: Centre of West African Studies, uk 34-56.
- Tsui, W. M. (2008). "Basotho Oral Poetry at the Beginning of the 21st Century". Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Afrika Kusini.
- White, L. (1989). "Poetic License: Oral Poetry and History". Katika K. Barber. na P. F. Farias, (Wah). *Discourse and it's Disguises: The Interpretation of African Oral Text*. Birmingham: Centre of West African Studies.